

**KUMB: PPR/17 - 10/1**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 4 OKTOBA 2017**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 4 Oktoba 2017**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 6 Septemba 2017. Kwa mwezi Oktoba 2017, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 74/lita (sawa na asilimia 3.72), Shilingi 21/lita (sawa na asilimia 1.11) na Shilingi 47/lita (sawa na asilimia 2.61) sawia. Vilevile, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 74.07/lita (sawa na asilimia 3.94), Shilingi 20.94/lita (sawa na asilimia 1.18) na Shilingi 47.22/lita (sawa na asilimia 2.78) sawia. Ongezeko la bei za mafuta kwenye soko la ndani, limetokana na ongezeko la bei za mafuta hayo katika soko la dunia na kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani, fedha inayotumika kununulia mafuta.
- (b) Hakuna mabadiliko ya bei za mafuta kwa **Mkoa wa Tanga** kwani hapakuwa na mzigo mpya wa mafuta uliopokelewa kwenye bandari ya Tanga kwa mwezi Septemba 2017. Kwa hivyo, bei za mafuta mkoani Tanga kwa mwezi Oktoba 2017, zitaendelea kuwa kama zilivyokuwa mwezi Septemba 2017.
- (c) Itakumbukwa ya kwamba, mwishoni mwa mwezi Agosti 2017, EWURA ilitoa taarifa na kuzishauri Kampuni za Uuzaji wa Mafuta ya Petroli kwa Jumla (OMCs) kuanza kuingiza mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kupitia bandari ya Tanga kwa kuwa kuanzia mwezi wa Oktoba 2017, mikoa ya Kaskazini yaani Arusha, Kilimanjaro na Manyara, itakuwa inapata mahitaji ya mafuta ya petroli kupitia bandari ya Tanga na kwamba, bei za mafuta yatakayouzwa katika mikoa hiyo ya Kaskazini zitakokotolewa kulingana na bei ya mafuta yaliyoagizwa nchini kupitia Bandari ya Tanga badala ya Bandari ya Dar es Salaam . Hii ni kutokana na kuimarika kwa miundo mbinu ya upakuaji wa mafuta ya petroli mkoani Tanga kupitia mfumo wa Uingizwaji wa Mafuta ya Petroli kwa Pamoja (BPS). Uamuzi huu umefanywa ili kuongeza ufanisi na usalama wa kupokea mafuta nchini na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata mafuta ya petroli kwa bei nafuu zaidi hasa kwa kupunguza gharama za usafirishaji. EWURA inapenda kuufahamisha umma ya kwamba, kutakuwa na mafuta ya kutosheleza mahitaji ya mkoaa wa Tanga na mikoa ya Kaskazini kwa mwezi wote wa Oktoba kwa kuzingatia kiasi cha mafuta kilichopo Tanga hivi sasa na kinachotegemewa kupokelewa katika Bandari ya Tanga mwanzoni mwa mwezi Oktoba.
- (d) Kutokana na maelezo ya kipengele (c) kwa mwezi Oktoba 2017, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kwa Mikoa ya Kaskazini ya Arusha, Kilimanjaro na Manyarea imepungua kuanzia Shilingi24/lita hadi Shilingi 31/lita (sawa na kuanzia asilimia 1.1% hadi 1.4%), Shilingi 38/lita hadi

Shilingi 45/lita (sawa na kuanzia asilimia 1.9% hadi 2.2%) na Shilingi 29/lita hadi Shilingi 36/lita (sawa na kuanzia asilimia 1.5% hadi 1.8%), sawia. Kupungua kwa bei za mafuta katika mikoa ya Kaskazini inatokana na kushuka kwa gharama za usafirishaji kutokana na uamuzi wa kupakia mafuta hayo kutoka Tanga badala ya Dar es Salaam, kama ilivyokuwa huko nyuma. Vilevile, bei za mafuta yaliyopo Tanga hazijabadilika kutokana na kuwa hakuna mzigo mpya uliopokelewa mwezi Septemba 2017 na hivyo bei za jumla za mafuta ya petroli mkoani Tanga zinabaki kuwa ni zile za Agosti 2017 zilizokokotolewa kwa kuzingatia bei ya mafuta ya petroli katika soko la dunia za mwezi Julai 2017.

- (e) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba **\*152\*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hiso zisivuke bei kikomo (*price cap*)** kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 216/2017 la mwezi Mei 2017.**
- (h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuvi wahakikishe wanapata stakabadhi hiso za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiso za malipo zitatumika kama kidhibiti cha wanunuvi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hiso zitasaidia kurahishisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mafuta ya petroli.

## A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
<b>Dar es Salaam</b>	<b>2,063</b>	<b>1,908</b>	<b>1,858</b>
<b>Arusha</b>	<b>2,049</b>	<b>1,933</b>	<b>1,866</b>
Arumeru (Usa West)	2,049	1,933	1,866
Karatu	2,067	1,951	1,884
Monduli	2,055	1,938	1,872
Monduli-Makuyuni	2,059	1,943	1,876
Ngorongoro (Loliondo)	2,134	2,017	1,951
<b>Kibaha</b>	<b>2,067</b>	<b>1,912</b>	<b>1,863</b>
Bagamoyo	2,074	1,919	1,869
Kisarawe	2,070	1,915	1,865
Mkuranga	2,073	1,918	1,868
Rufiji	2,091	1,935	1,886
<b>Dodoma</b>	<b>2,122</b>	<b>1,966</b>	<b>1,917</b>
Bahi	2,129	1,974	1,924
Chemba	2,148	1,993	1,943
Kondoa	2,154	1,999	1,949
Kongwa	2,119	1,964	1,914
Mpwapwa	2,123	1,968	1,918
<b>Iringa</b>	<b>2,127</b>	<b>1,972</b>	<b>1,922</b>
Kilolo	2,131	1,976	1,927
Mufindi (Mafinga)	2,137	1,982	1,932
<b>Njombe</b>	<b>2,155</b>	<b>2,000</b>	<b>1,950</b>
Ludewa	2,193	2,038	1,988
Makete	2,186	2,031	1,981
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,153	1,998	1,948
<b>Bukoba</b>	<b>2,278</b>	<b>2,123</b>	<b>2,073</b>
Biharamulo	2,252	2,097	2,047
Karagwe (Kayanga)	2,294	2,139	2,089
Kyerwa (Ruberwa)	2,300	2,145	2,095
Muleba	2,278	2,123	2,073
Ngara	2,243	2,088	2,039
Misenyi	2,286	2,131	2,081
<b>Geita</b>	<b>2,228</b>	<b>2,073</b>	<b>2,023</b>
Bukombe	2,217	2,062	2,012
Chato	2,249	2,094	2,044
Mbogwe	2,266	2,111	2,061
Nyang'hwale	2,243	2,088	2,038
<b>Kigoma</b>	<b>2,294</b>	<b>2,139</b>	<b>2,089</b>

Uvinza (Lugufu)	2,306	2,151	2,101
Buhigwe	2,283	2,128	2,078
Kakonko	2,251	2,096	2,046
Kasulu	2,280	2,125	2,075
Kibondo	2,258	2,103	2,053
<b>Moshi</b>	<b>2,039</b>	<b>1,923</b>	<b>1,856</b>
Hai (Bomang'ombe)	2,042	1,926	1,859
Mwanga	2,032	1,916	1,849
Rombo (Mkuu)	2,056	1,939	1,873
Same	2,025	1,909	1,842
Siha (Sanya Juu)	2,045	1,929	1,862
<b>Lindi</b>	<b>2,122</b>	<b>1,967</b>	<b>1,917</b>
Lindi-Mtama	2,140	1,985	1,935
Kilwa Masoko	2,097	1,942	1,892
Liwale	2,143	1,987	1,938
Nachingwea	2,151	1,996	1,946
Ruangwa	2,152	1,997	1,948
<b>Babati</b>	<b>2,083</b>	<b>1,967</b>	<b>1,900</b>
Hanang (Katesh)	2,094	1,978	1,911
Kiteto (Kibaya)	2,098	1,982	1,915
<b>Mbulu</b>	<b>2,096</b>	<b>1,980</b>	<b>1,913</b>
Simanjiro (Orkasumet)	2,115	1,999	1,932
<b>Musoma</b>	<b>2,241</b>	<b>2,086</b>	<b>2,036</b>
Musoma Vijijini (Busekela)	2,282	2,127	2,077
Rorya (Ingirijuu)	2,250	2,095	2,045
Rorya (Shirati)	2,285	2,129	2,080
Bunda	2,232	2,077	2,027
Butiama	2,238	2,083	2,033
Serengeti (Mugumu)	2,287	2,131	2,082
Tarime	2,252	2,097	2,047
<b>Mbeya</b>	<b>2,170</b>	<b>2,015</b>	<b>1,965</b>
Chunya	2,179	2,024	1,974
Chunya (Makongolosi)	2,193	2,038	1,989
Ilaje	2,183	2,028	1,978
Kyela	2,186	2,030	1,981
Mbarali (Rujewa)	2,154	1,999	1,949
Mbozi (Vwawa)	2,179	2,024	1,974
Momba (Chitete)	2,188	2,033	1,983
Rungwe (Tukuyu)	2,179	2,024	1,974
<b>Morogoro</b>	<b>2,088</b>	<b>1,933</b>	<b>1,883</b>
Mikumi	2,104	1,948	1,899
Kilombero (Ifakara)	2,126	1,970	1,921
Kilombero (Mlimba)	2,148	1,993	1,943
Kilombero (Mngeta)	2,137	1,982	1,932
Ulanga (Mahenge)	2,136	1,981	1,931

Malinyi	2,146	1,991	1,942
Kilosa	2,106	1,951	1,901
Gairo	2,106	1,951	1,901
Mvomero (Wami Sokoine)	2,098	1,943	1,894
Turiani	2,113	1,958	1,908
<b>Mtwara</b>	<b>2,135</b>	<b>1,980</b>	<b>1,930</b>
Nanyumbu (Mangaka)	2,184	2,029	1,979
Masasi	2,161	2,006	1,956
Newala	2,167	2,012	1,962
Tandahimba	2,160	2,005	1,955
<b>Mwanza</b>	<b>2,213</b>	<b>2,058</b>	<b>2,008</b>
Kwimba	2,249	2,094	2,044
Magu	2,221	2,066	2,016
Misungwi	2,218	2,063	2,013
Sengerema	2,245	2,090	2,040
Ukerewe	2,272	2,117	2,067
<b>Sumbawanga</b>	<b>2,235</b>	<b>2,080</b>	<b>2,031</b>
Kalambo (Matai)	2,228	2,073	2,023
Nkasi (Namanyele)	2,249	2,094	2,044
Katavi (Mpanda)	2,270	2,115	2,066
Mlele (Inyonga)	2,249	2,094	2,044
<b>Songea</b>	<b>2,186</b>	<b>2,031</b>	<b>1,981</b>
Mbinga	2,220	2,064	2,015
Namtumbo	2,215	2,060	2,011
Nyasa (Mbamba Bay)	2,222	2,067	2,017
Tunduru	2,245	2,090	2,040
<b>Shinyanga</b>	<b>2,192</b>	<b>2,036</b>	<b>1,987</b>
Kahama	2,205	2,050	2,000
Kishapu	2,220	2,065	2,015
Simiyu (Bariadi)	2,233	2,078	2,028
Busega (Nyashimo)	2,226	2,071	2,021
Itilima (Lagangabilili)	2,236	2,081	2,031
Maswa	2,224	2,069	2,020
Meatu (Mwanhuzi)	2,231	2,076	2,027
<b>Singida</b>	<b>2,153</b>	<b>1,998</b>	<b>1,949</b>
Iramba	2,166	2,010	1,961
Manyoni	2,138	1,983	1,933
Ikungi	2,149	1,994	1,944
Mkalama (Nduguti)	2,178	2,023	1,973
<b>Tabora</b>	<b>2,217</b>	<b>2,062</b>	<b>2,012</b>
Igunga	2,171	2,016	1,966
Kaliua	2,235	2,080	2,030
Ulyankulu	2,229	2,074	2,024
Nzega	2,181	2,026	1,977
Sikonge	2,229	2,073	2,024

Urambo	2,230	2,075	2,025
<b>Tanga</b>	<b>1,993</b>	<b>1,877</b>	<b>1,810</b>
Handeni	2,013	1,897	1,830
Kilindi	2,028	1,912	1,845
Korogwe	2,005	1,889	1,822
Lushoto	2,014	1,898	1,831
Mkinga (Maramba)	2,000	1,884	1,817
Muheza	1,998	1,881	1,814
Pangani	1,999	1,883	1,816

### B: BEI ZA JUMLA

<b>Bei za Jumla – DSM</b>	<b>Petroli (Shs/Lita)</b>	<b>Dizeli (Shs/Lita)</b>	<b>Mafuta ya Taa (Shs/Lita)</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>1,951.95</b>	<b>1,796.79</b>	<b>1,747.14</b>

<b>Bei za Jumla - TANGA</b>	<b>Petroli (Shs/Lita)</b>	<b>Dizeli (Shs/Lita)</b>	<b>Mafuta ya Taa (Shs/Lita)</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>1,881.70</b>	<b>1,765.56</b>	<b>1,698.68</b>

**Mhandisi Godwin Samwel**  
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**  
**EWURA**